OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA MUFINDI

SHULE YA SEKONDARI KIBENGU,

S.L.P 360,

**MAFINGA**

13.12.20

MWANAFUNZI………………………………………….

KIJIJI CHA…………………………………………………

**MAFINGA.**

YAH: **MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE HII MWAKA 2021**

- Nafurahi kukutaarifu kuw a**umechaguliwa kujiunga kidato cha kwanza** katika shule hii.
- **Masomo yote** katika shule hii yanafundishwa kwa lugha ya **kiingereza** isipokuwa somo la Kiswahili. Hivyo unatakiwa kujibidiisha sana katika kuelewa somo la Kiingereza daima uwapo maeneo ya shule. Aidha unashauriwa kuwa na **kamusi ya Kiingereza** (Dictionary) kwa msaada zaidi
- **Tarehe ya kufungua shule**. Shule itafunguliwa tarehe **11/01/2021 saa 1:00**asubuhi. Siku hiyo walimu wataanza kufundisha **kozi ya kiingereza** (English orientation course).

- **SARE YA SHULE**
  - **WAVULANA**.
    - Suruari ya rangi ya damu ya mzee moja(1) na rangi ya kijani moja(1)).
    - Mashati meupe mikono mifupi mawili (2)
    - Tai mbili (2)za rangi za suruari
    - Soksi nyeusi jozi mbili (2)
    - Viatu vyeusi vya ngozi, vya kamba vya kung’arisha, jozi mbili (2)
    - Sweta damu ya mzee moja (1) na kijani moja (1)
    - Mashuka mawili (2) yapinki, blanketi moja na godoro dogo
  - **WASICHANA**
    - Sketi mbili (2), kijani moja na damu ya mzee moja)
    - Blauzi mbili (2) nyeupe za mikono mifupi
    - Tai mbili za rangi za sketi

- Soksi nyeupe jozi mbili (2)
- Viatu vyeusi vya ngozi, vya kung'arisha jozi mbili (2)
- Sweta mbili, damu ya mzee moja na kijani moja
- Mashuka mawili (2) ya pinki, blanketi moja na godoro dogo

- **VIFAA VINGINE**

- Daftari kubwa (kaunta) 10 (2 quire au 3 quire) za kuanzia, kalamu, rulan.k.
- Daftari ndogo za Msomi kwa ajili ya mazoezi
- Mathematical set (mkebe wenye vifaa) na rula moja ya cm thelathini
- Vifaa kwa ajili ya usafi binafsi kama ndoo, beseni, sabunin.k
- Kamusi ya Kiingereza-Kiswahili
- Rim moja A4 kwa ajili ya mitihani na majaribio (makubaliano ya wazazi

- **SHERIA NA KANUNI ZA SHULE.**

Shule hii inaongozwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yatafafanuliwa vizuri mara baada ya kuwasili shuleni:

- Heshima kwa viongozi, walezi, wafanyakazi na wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima
- Mahudhurio katika shughuli za nje na ndani ni lazima
- Kutimiza kwa ujumla maandalio ya jioni (evening preparation)
- Ni lazima kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa
- Ni lazima kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ama ya kuwepo ndani ya shule au nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uwanafunzi wako
- Ni lazima kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule
- Ni lazima kuvaa sare ya shule wakati wote unaotakiwa
- Ni lazima kuzingatia ratiba ya shule

- **MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE**
  - Wizi
  - Uasherati, ubakaji na ushoga
  - Ulevi na matumizi ya dawa za kulevya
  - Makosa ya jinai
  - Kupiga au kupigana
  - Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
  - Kuharibu bendera ya taifa
  - Kuoa au kuolewa
  - Kupatamimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule
  - Kutoa mimba
  - Kugoma, kuchochea au kuongoza migomo au kuvuruga amani na usalama wa shule
  - Kukataa adhabu kwa makusudi
  - Kumiliki simu

**MUHIMU**:

**Mwanafunzi aletwe shuleni na mzazi au mlezi mwenyewe siku ya kufungua shule**

**TAFADHALI SOMA MAELEKEZO HAYA KWA MAKINI NA KUYATEKELEZA**
**KARIBU SANA KATIKA SHULE HII YA KIBENGU SEKONDARI**

_________________

**JOHN JOHN MUTUGUMONGA**
**MKUU WA SHULE**

KIAMBATA (A)

……………………………………

………………………………………

………………………………………

MKUU WA SHULE,

SHULE YA SEKONDARI KIBENGU,

S.L.P 360,

MAFINGA.

YAH: KUKUBALI KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI KIBENGU MWANAFUNZI……………………………………………………………………………..

KIDATO CHA _______________MWAKA___________

1. Mimi…………………………………………… Mzazi/mlezi wamwanafunzi aliyetajwa hapo juu, ninakiri kuwa nimeyaelewa maelezo yote (joining instruction) yaliyotolewa.

2. Ninakubali mwanangu aendelee na masomo, na nitatekeleza yote yale yanayonihusu kwa wakati wake, kama ilivyoagizwa katika maelezo ya kujiunga nas hule hii.

3. Naahidi kumhudumia mtoto wangu kwa hali na mali ili kufikia malengo yake ya kujiunga na shulehii.

4. Naahidi Kufuatilia/kusimamia nidhamu na maendeleo yake muda wote awapo hapo shuleni.

JINA LA MZAZI/MLEZI…………………………………………………………………

SAHIHI YAKE……………………………………………………

Nambaya simu…………………………………………………….

Mimi…………………………………………ninakubali kwa hiari yangu kujiunga na shule hii, naahidi kuwa mtiifu wa sheria za shule, kuwa na nidhamu, kusoma kwa bidii, na kuwa mfano wa kuigwa kwa wanafunzi wenzangu ili nifikie malengo yangu ya kujiunga na shule hii.

JINA LA MWANAFUNZI…………………………………………………………

SAHIHI…………………………………………………

MAELEZO MENGINE MUHIMU KUZINGATIA

1. Kila mzazi/mlezi na mwanafunzi kujaza **kiambata A** na kukileta siku inapofungua shule
2. Mzazi/mlezi **amlete mtoto kwa wakati uliopangwa** hata kama hajakamilisha mahitaji ataendelea kumkamilishiwa wakati mtoto anaendelea na masomo.Mwisho wa kuripoti shuleni ni tarehe 15/01/2021
3. Mzazi/mlezi hakikisha umempeleka mtoto kupima afya na daktari amejaza kiambata B
4. Kila mwanafunzi analazimika kutii na kuheshimu na kujua wimbo wa shule,wimbowaTaifa,Tanzania Tanzania nakupenda, naTazama Ramani
5. Cheti cha kuzaliwa (kivuli chake aje nacho)

…………………………..

JOHN JOHN MUTUGUMONGA

MKUU WA SHULE

KIAMBATA(B)

SHULE YA SEKONDARI KIBENGU,

S.L.P 360,

MAFINGA.

13/12/20

DAKTARI………………………………………………………….

HOSPITALI YA………………………………………………….

S.L.P…………………………………………………………………

FOMU YA KUPIMWA AFYA MWANAFUNZI.

Tafadhali naomba umpime mwanafunzi aliyetajwa hapo juu kwa gharama za mzazi wake, na uthibitishe kama ataweza kumudu masomo ya sekondari shule hii. Ni muhimu apimwe kabla ya kuja hapa shuleni kuanza masomo ya kidato cha kwanza-2021.

……………………………………

J.J. MUTUGUMONGA

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI KIBENGU,

S.L.P 360,

MAFINGA

15/12/2019

YAH: MWANAFUNZI.........................................................................................................

UMRI…………………………………..

Matokeo ya vipimo vya afya ya mwanafunzi aliyetajwa hapo juu.

1. Blood comment (red & white)……………………………………………..
2. Urine……………………………………
3. Stool……………………………………..
4. Pregnancy test………………………………
5. BP test……………………………………
6. Ear test…………………………………..
7. Eye test…………………………………..
8. Spleen……………………………………
9. Additional information,any other physical,hereditary or infectious diseases……………………………………………………………………………………..

Nathibitishakuwamwanafunzihuyu................................................ ataweza/hataweza kumudu masomo ya sekondari kwa sababu: .........................................................................................................................................

........................................................................................................................................

JINA LA DAKTARI ……………………………………………SAHIHI………………………………

CHEO/WADHIFA……………………………TAREHE………………….MUHURI